JINSI YA KUSAIDIA

HUZUNI . . . . . . ULEVI

UGONJWA . . . . UASHERATI

NJAA . . . . SHETANI

UTASA . . . . UCHAWI

HAROLD CUMMINS

Kuwa mzee ni mpango wa Mungu. Soma Zaburi 71:17-18.

Miaka ya uzee yaweza kuwa wakati mzuri. Soma Zaburi 91:14-16.

- — Wakati wa hekima .... Yohana 12:12
- — Uzuri wa kiroho .... Mithali 16:31
- — Mazao ya wakati wa uzee .... Zaburi 92:12-15
- — Kuishi kwa hekima .... Zaburi 90:12
- — Hekima na Uzee .... Mithali 3:16-18
- — Nafasi ya kufundisha .... Zaburi 34:11-14
- — Watoto yawapasa kuwasaidia wazazi wao .... 1 Timotheo 5:4
- — Ahadi ya Kristo .... Yohana 14:1-6

■ WASIWASI .... Kusumbuliwa, dhiki, kukata tamaa na hofu.
Wasiwasi huondolewa na imani. Soma Zaburi 37:1-5.

Ishi leo bila hafu kuhusu kesho. Soma Mathayo 7:25-34.

- — Msaada kutoka kwa Roho Mtakatifu .... Marko 13:11
- — Kutazama juu .... Luka 21:25-28
- — Kuongozwa na Mungu .... Warumi 8:28
- — Kusaidiwa na maombi .... Wafilipi 4:6
- — Utajiri wa Roho .... 2 Wakorintho 6:10
- — Omba nawe utapata .... Luka 11:9-11
- — Matunzo ya Mungu .... 1 Petro 5:6-7

Tazama katika kitabu hiki: "Mimi sina furaha." Pia tazama: "Mateso."

■ WATOTO .... Shida za wazazi na watoto.
Watoto ni vipawa kutoka kwa Mungu. Soma Mwanzo 33:5.

Wajibu wa wazazi. Soma Waefeso 6:1-4.

- — Penda watoto wako .... Tito 2:4
- — Mpe Mungu watoto wako .... 1 Samweli 1:24
- — Mwongoze kila mtoto kwa Yesu .... Mathayo 19:13-14
- — Fundisha juu ya Mungu .... Kumbukumbu la Torati 6:4-7
- — Usiwachokoze .... Wakolosai 3:21
- — Msaada kutoka kwa Mungu .... Wafilipi 4:6-7

Soma katika kitabu hiki: "Watoto wetu si Wakristo waaminifu," "Ndoa yetu ina shida." Pia Tazama: "Utasa."

■ ZINAA .... Tazama "Binti yetu ana mimba lakini hajaolewa."
Pia tazama: "Uasherati."

JINSI YA KUSAIDIA

Kitabu cha Kuwaongoza Watu Wanaowasaidia Wengine

Kimeandikwa

na

Harold Cummins

© Copyright. 1998. 2004
Kenya Baptist Media
All Rights Reserved

**Kimetolewa na Kuchapwa na
Kenya Baptist Media
Thika Road, Ruaraka
Box 30370, Nairobi**

— Acha hasara hii na Mungu .... Ayubu 5:8-11
— Njia ya kufariji .... Yohana 14:18-20, 25-28
— Tafuta utunzaji wa kanisa lako .... 1 Timotheo 5:3-16
— Omba na utapata .... Luka 11:9-11

Soma katika kitabu hiki: "Tumefiwa katika jamaa yetu." Pia angalia: "Shida", "Huzuni" na "Uzee."

■ ULEVI .... Tazama katika kitabu hiki: "Mume wangu hunywa pombe sana."

Pia tazama kuhusu: "Mkristo kurudi nyuma," "Shida" na "Huzuni."

■ UMASKINI .... Tazama katika kitabu hiki: "Twahitaji chakula na pesa." Pia angalia: "Kukosa kazi," na "Shida."

■ UNYONGE .... Kuwa bila nguvu.

Nguvu za Mungu hutimilika katika udhaifu. Soma 2 Wakorintho 12:8-10.

Nguvu zapatikana na kuweka dhambi kando. Soma Waebrania 12:1

— Kutoamini kwatunyang'anya nguvu .... Mathayo 17:19-20
— Tumia silaha za Mungu .... Waefeso 6:10-17
— Roho wa Mungu ana nguvu .... 1 Yohana 4:4
— Nguvu ni za Mungu .... Zaburi 26:11
— Mungu anaweka uweza ndani yako .... 2 Wakorintho 13:3-4
— Sifu nguvu za Mungu .... Zaburi 21:31
Nguvu kutoka katika udhaifu .... Waebrania 11:32-34

Tazama pia: "Hofu" na "Huzuni."

■ UTASA .... Kutopata mimba na kutozaa

Uvumilivu mpaka Mungu awe tayari. Soma Mhubiri 7:8.

Mara nyingi imani tu katika Mungu husaidia. Soma Waebrania 11:11.

— Kipawa cha Mungu katika wakati wake .... 1 Samweli 1:11-20
— Pengine ni jaribio la imani .... Yakobo 1:2-4
— Uvumilivu wenye furaha .... Wakolosai 2:11-12
— Bwana hupeana .... Ayubu 1:21
— Kupokea ahadi kwa imani .... Waebrania 11:32-34
— Kuwa katika hali ya kuridhika .... Wafilipi 4:11-12

Tafuta pia katika kitabu hiki: "Wasiwasi" na "Mateso."

■ UZEE .... Hali ya kuzeeka

- **UCHAWI** .... **Soma katika kitabu hiki: "Kijana wetu anazungumza upuzi - Je, amerogwa?" Soma pia: Kumbukumbu la Torati 18:9-14; Mika 5:12; Wagalatia 5:20; na Waefeso 6:11. Pia tazama: Shetani."**
- **UCHUNGU .... Chuki, maudhiko, na uadui. Uchungu huleta shida. Soma Waebrania 12:15. Jibu ni msamaha. Soma Mathayo 18:21-22.**

  - — Maneno yenye uchungu .... Zaburi 64:3-4
  - — Onyo na suluhisho .... Waefeso 4:31-32
  - — Hatari ya chuki .... Mithali 26:24-26
  - — Jibu la Yesu .... Yohana 13:34-35
  - — Rudisha upendo badala ya chuki .... Mathayo 5:38-41
  - — Kusameheana .... Wakolosai 3:12-15

Tazama pia katika kitabu hiki: "Mimi nina hasira sana."

- **UDHALIMU .... Tendo la kufanya maonevu, kuwaonea na kuwapendelea wengine.**

Heri ni kwa wale wanaoumia kwa udhalimu. Soma Mathayo 5:11-12.

Mgeukie Mungu unapotendewa mabaya. Soma Waebrania 4:15-16.

  - — Kristo ndiye mfano wetu .... Wafilipi 2:3-8
  - — Mungu ndiye usalama wetu .... Zaburi 23:1
  - — Mungu ndiye nguvu yetu .... Kumbukumbu la Torati 33:27
  - — Kristo yuko pamoja nawe .... Mathayo 18:20
  - — Mpe Mungu mzigo wako .... Zaburi 55:22
  - — Fanya yaliyo haki wewe mwenyewe .... Mika 6:8

Tafuta pia katika kitabu hiki kuhusu: "Uchungu" na "Chuki."

- UGOMVI .... Tazama katika kitabu hiki "Mimi nimekasirika sana." Na pia tazama: "Uchungu."
- UGONJWA .... Soma katika kitabu hiki: "Mimi ni mgonjwa."
- UJANE .... Hali ya mtu kukaa bila mke au mume baada ya kufiwa.

Tafuta faraja katika neno la Mungu. Soma Isaya 54:4

Tafuta nguvu kwa ajili ya upweke wako. Soma Warumi 8:35-37.

  - — Kusikia huzuni katika hali ya ujane ni kawaida .. Ayubu 19:13-15

YALIYOMO

SEHEMU YA 1 MFANO NA KANUNI 6
Jinsi ya kutumia kitabu hiki na jinsi utakavyoanza kuwasaidia wengine.

SEHEMU YA 2. KUWASAIDIA WENYE SHIDA 14
Njia za kuwashauri watu walio na matatizo, hatua kwa hatua.

SEHEMU YA 3 MAJIBU YA MUNGU KWA TAABU ZETU 40
Shida nyingine, na vifungu vya Biblia.

Njia za kupokea na kutoa msaada kutoka katika Biblia.

Kitabu hiki kimetafsiriwa na
Joe Michael Kamau

DIBAJI

"Mume wangu amekutana na mwanamke mwingine huko mjini. Sasa wanakaa pamoja! Kwa nini mume wangu ananifanyia hivi? Tuna watoto watano, na mimi ni Mkristo mwaminifu. Nitafanya nini niweze kuokoa ndoa yetu?" Je, mke huyo atafanya nini? Ungeweza kumsaidia kwa njia gani?

"Binti yetu huumwa sana na kichwa. Anakaa usiku kucha bila kulala, huku akipiga kelele na kupayuka maneno ovyo ovyo. Wakati mwili wake unapopatwa na maumivu, yeye huanza kujitupatupa huko na huko na kupigana na ye yote aliye karibu naye. Mwishowe huanza kulegea na hata kupotelewa na fahamu. Ndugu zetu wanaamini ya kwamba ni uchawi. Waweza kutusaidia?" Je, unaweza kutatua shida hii namna gani?

"Mtoto wetu wa pekee alikufa mwezi uliopita. Tangu mtoto huyo azaliwe, miaka saba iliyopita, mke wangu amekuwa tasa. Tumejaribu kupata watoto wengine, bila kufaulu. Wazazi wangu wanasisitiza nioe mke wa pili. Lakini, mimi kama Mkristo, naona ni kosa kuoa mke wa pili. Nifanye nini?" Je, unaweza kusaidia jamii hii?

Katika mji au kijiji mahali unakokaa, watu wengi wana shida kama hizo. Ugonjwa, utasa, kupeana talaka, uchawi, na ukosefu wa kazi ni shida ambazo zinawakabili watu siku hizi. Wao hujisikia kuwa na huzuni, hofu, hasira, uchungu, hatia na wasiwasi.

Kitabu hiki kitakusaidia katika shida nyingi. Makusudi ya kitabu hiki ni kama yafuatayo:

A) kukusaidia kuelewa zaidi shida za watu,

B) kukusaidia kujifunza njia maalum za kusaidia watu kutatua taabu zao,

C) kukusaidia kupata msaada kwa haraka katika Biblia juu ya shida zile kubwa.

Kwa hiyo, kitabu hiki cha mwongozo ni kwa ajili ya viongozi Wakristo wanaotaka kuwasaidia watu kutatua shida zao.

TAZAMA: Miraba na miviringo inasaidia kuonyesha jinsi ya kutumia kitabu hiki. Kila mraba ■ unaonyesha shida. Na kila mviringo ● ni sehemu ya jibu kutoka katika Biblia.

Tazama pia katika kitabu hiki: "Tumefiwa katika jamaa yetu." "Ndoa yetu ina shida." Pia tazama: "Wasiwasi."

■ SHIDA ZA JAMAA . . Soma katika kitabu hiki "Ndoa yetu ina shida," "Watoto wetu si Wakristo waaminifu," "Mume wangu na kijana wetu si Wakristo." Pia tazama: "Watoto na shida."

■ TALAKA .... Tafuta: "Ndoa yetu ina shida". Pia angalia: "Shida" na "kuoa mke zaidi ya mmoja."

■ UADUI .... Angalia katika kitabu hiki: "Mimi nimekasirika sana," Pia angalia: "Chuki" na "Uchungu."

■ UASHERATI .... Kujuana kimwili nje ya ndoa. Usinzi (Kutoka 20:14).

Yesu akamwambia, "Wala mimi sikuhukumu. Enenda zako, wala usitende dhambi tena" (Yohana 8:11).

— Uasherati ni kosa kubwa .... Mithali 6;32
— Mungu atahukumu .... Waebrania 13:4
— Upendo ndio jibu .... Waefeso 5:28-29; Tito 2:4-5
— Msamaha wa dhambi .... Waefeso 1:7
— Mungu anaweza kukusafisha .... 1 Yohana 1:9
— Msamaha wa uasherati .... Zaburi 51:1-3
— Mwanzo mpya .... Wafilipi 3:13-14

Tazama pia katika kitabu hiki: "Binti yetu ana mimba," "Nimetenda dhambi kubwa," "Ndoa yetu ina shida," "Nina tamaa kubwa zisizo za Kikristo."

■ UBAGUZI .... Kiburi, dhuluma, ukabila, na kuwaonea na kuwapendelea watu wengine.

Mpango wake Yesu kushinda ubaguzi. Soma Mathayo 5:38-48.

Mtendee kila mmoja kama ndugu yako. Soma Warumi 14:10-13 na Yakobo 2:1-4.

— Jinsi ubaguzi unapofanya kazi .... 1 Yohana 2:9-11
— Usihukumu .... Luka 6:37-38
— Kushinda kwa ubaguzi .... Mathayo 7:12
— Upendo ndio jibu la ubaguzi .... 1 Yohana 4:11-12
— Njia ya Mungu ya kutoka katika ubaguzi .... Yakobo 4:8

Tazama pia: "Uchungu" na "Mateso."

— Mungu na Neno lake .... Mitume 20:32
— Nguvu katika maombi .... 1 Wathesalonike 5:16-18
— Kukaa katika Kristo .... Yohana 15:4-9
— Kuimarishwa katika ukweli .... Waefeso 4:13-16
— Kutumia silaha za Mungu .... Waefeso 6:10-20
— Ahadi ya Mungu .... Yohana 10:27-29

Tazama pia katika kitabu hiki: "Watoto wetu si Wakristo waaminifu."

■ NDOA Tazama: .... "Tunataka kuoana, "Ndoa yetu ina shida."
Pia angalia: "Watoto" na "Kuoa mke zaidi ya mmoja."

■ NGONO .... Tazama: "Ndoa yetu ina shida," "Binti yetu ana mimba," na "Twataka kuoana," "Uasherati," na "Utasa."

■ NJAA .... Tazama: "Twahitaji chakula na pesa."
Pia angalia: "Wasiwasi."

■ SHETANI .... yule mwovu aliyekataa kufuata amri ya Mungu. Elewa tabia yake. Soma Luka 8:29; Waefeso 2:2; Yakobo 4:7.

Ujue kusudi lake. Soma Marko 4:15; Ayubu 2:4-5; Luka 4:6-8.

— Ndiye anayetushtaki .... Ufunuo 12:10
— Nguvu za Shetani kwa wasioamini .... Yohana 8:44
— Nguvu yake si nyingi kwa Wakristo .... 2 Wakorintho 11:14-15
— Ushindi wa Kristo juu ya Shetani .... Marko 3:25-27
— Mkristo amshinda Shetani .... Yakobo 4:7
— Upigane na Shetani .... Waefeso 6:11-16
— Umshinde Shetani .... Ufunuo 12:10-11

"Kijana wetu anazungumza upuzi," na "Nimetenda dhambi kubwa".
Pia tazama: "Hofu" na "Dhambi."

■ SHIDA .... Taabu kubwa, sikitiko, msiba, dhiki. Mungu atakupatia nguvu za kiroho. Soma Zaburi 3:1-6. Unaweza kuvumilia wakati wa msiba. Soma 1 Wakorintho 10:13.

— **Kristo ndiye mshindi wa maovu** .... **Waebrania 13:6**
— **Mungu hatakuacha** .... **Kumbukumbu la Torati 31:8**
— **Nguvu kwa kila jambo** .... **Wafilipi 4:13**
— **Omba msaada** .... **Zaburi 34:6**
— **Msaada wa msaidizi** .... **Yohana 14:26**
— **Mngojee Bwana** .... **Isaya 40:29-31**

ORODHA YA KUKUSAIDIA KUPATA MSAADA HARAKA

SOMO	UKURASA	SOMO	UKURASA
Chuki	14, 15, 41	Njaa	28, 29, 44
Dhambi	22-25, 38	Ngono	24-27, 44
Furaha	18, 19	Pesa	28, 29
Hasira	14, 15	Shetani	34, 35
Hatia	22, 23, 41	Shida	6,7, 17, 45
Hofu	18, 19, 41	Shida za Jamii	20, 21, 36-39
Huzuni	18, 19, 42	Talaka	20, 21, 45
Kanisa	32, 38, 39	Uadui	14, 15, 45
Kifo	6, 7, 42	Uasherati	22-25
Kukata tamaa	18, 19, 42	Ubaguzi	45
Kukua Kikristo	38, 39	Uchawi	34, 35, 46
Kuoa wake wawili	42	Uchungu	14, 15, 46
Kukosa kazi	28, 29, 43	Udhalimu	46
Kushindwa	20	Ugomvi	14, 15, 46
Kushuhudia	36, 37	Ugonjwa	16, 17
Majaribu	26, 27	Ujane	6, 7, 46-47
Maradhi	16, 17	Ulevi	26, 27, 30, 31
Masikitiko	6, 7, 18, 19	Umaskini	28, 29, 47
Mateso	18, 19	Unyonge	47
Maumivu	16, 17	Utasa	47
Mazoea mabaya	26, 27, 30, 31	Uzee	48
Mimba	24, 25, 43	Wasiwasi	18, 19, 48
Mkristo kurudi nyuma	38, 39	Watoto	38, 39, 48
Ndoa	20, 21, 32, 33	Wokovu	36, 37
		Zinaa	22-25

SEHEMU YA 1 — MFANO NA KANUNI

Katika ukurasa wa kushoto, kuna mashauri ya kumsaidia mtu mwenye shida fulani. Katika ukurasa wa kulia, kuna vifungu vya Biblia vyenye msaada.

MFANO

"TUMEFIWA KATIKA JAMAA YETU."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Nenda mara moja kwa wale waliofiwa. Unahitajika huko kama rafiki Mkristo.
2. Sikiliza wale walio na huzuni. Sikiliza kwa moyo unaojali. Wakumbushe kwa upole watu hao ya kwamba Mungu atosheleza mambo yote.
3. Ikiwa yule aliyekufa alikuwa Mkristo, unaweza kuwakumbusha hao walio na huzuni ya kwamba roho ya mpendwa wao sasa iko pamoja na Mungu. Huyo aliyekufa ameyaacha maumivu na sasa anayo furaha tele.
4. Ikiwa aliyekufa hakuwa Mkristo, pia inawezekana kufariji walio na huzuni kwa kuwasikiliza katika upendo wa Kikristo. Unaweza kuongea kwa kifupi juu ya upendo wa Mungu, na kusoma vifungu vya Biblia kama Zaburi 27:7-11 na 2 Petro 3:8-14.
5. Ikiwa umeombwa, unaweza kusaidia katika mazishi. Tayarisha mahubiri kutoka katika Biblia. Watu wanahitaji Neno la Mungu kuhusu uhai na kifo.
6. Endelea kusaidia wale ambao maisha yao yamehuzunishwa na kifo. Unaweza kusaidia wakati wanapokata mashauri.
7. Waongoze walio na huzuni katika mabadiliko yo yote. Wanahitaji kutazamia maisha katika siku za usoni kwa imani. Pia wanahitaji kupanga mipango yao kulingana na Neno la Mungu. Wasaidie kutafuta furaha katika huzuni, wakijua baraka za kifo kwa Wakristo, na nguvu za Mungu katika maisha ya mtu.

— Uwe na matumaini na imani .... Warumi 15:13
— Upate maarifa mapya .... Mithali 4:4-5; 6:6-11
— Usiwe mvivu .... Warumi 12:11
— Mungu atakuwa pamoja nawe .... Zaburi 23:1-6

Toa mashauri yafuatayo: Tumia wakati wako kwa masomo ya Biblia kwa njia ya Posta (Bible Way Correspondence Course), kazi ya kanisa ya kujitolea, n.k. Tazama: "Twahitaji chakula na pesa." Pia angalia: "Shida," "Udhalimu," na "Huzuni."

■ MAJARIBU. .... Tazama: "Nina tamaa kubwa zisizo za Kikristo."

■ MASIKITIKO .... Tazama katika kitabu hiki: "Tumefiwa katika jamaa yetu." Pia tazama: "Wasiwasi" na "Hofu."

■ MATESO .... Shida, taabu, majaribu na matatizo.

Hakuna kinachoweza kututenga na upendo wa Mungu (Warumi 8:38-39). Omba na unyenyekee mbele za Mungu (2 Mambo ya Nyakati 33:12-13).

— Mateso hutusukuma kwa Neno la Mungu . Kumbukumbu la Torati 8:2-3
— Mateso hututoa makosa na kutuadilisha .... Waebrania 12:5-11
— Kuthibitisha imani yetu .... 1 Petro 1:5-8
— Uwe na furaha katika majaribu .... Yakobo 1:2-4
— Furahi katika maumivu .... Warumi 5:3-4
— Mungu hutoa msaada .... Zaburi 34:19
— Uvumilifu katika mateso .... Zaburi 130:1-6

Tazama pia katika kitabu hiki: "Mimi sina furaha," na "Mimi ni mgonjwa". Pia angalia "Wasiwasi."

■ MAUMIVU .... Soma katika kitabu hiki: "Mimi ni mgonjwa."

■ MIMBA .... Tazama: "Binti yetu ana mimba". Pia tafuta: "Utasa."

■ MKRISTO KURUDI NYUMA Kumwacha Mungu, na kuwa bila imani.

Kurudi nyuma katika Ukristo huja kutokana na imani isiyo ya kweli. Soma 2 Timotheo 3:8-9.

Neno la Mungu ndilo ngao. Soma 2 Timotheo 3:13-17.

— Kukua kiroho .... 2 Petro 1:5-9

— Mwamini Mungu .... Mithali 29:25

Tazama pia katika kitabu hiki: "Wasiwasi" na "Shida".

■ HUZUNI .... Sikitiko kubwa, kutokuwa na furaha, kutokuwa na tumaini.

Neema ya Mungu yatosha. Soma 2 Wakorintho 12:9.

Msingi wa furaha yako awe matumaini katika Kristo. Soma Warumi 12:12.

— Unaweza kushinda .... Ayubu 23:8-10
— Mkono wa Mungu waponya .... Ayubu 5:17-18
— Furaha ya Bwana .... Nehemia 8:9-10
— Tosheka katika maisha .... Wafilipi 4:11
— Furahi katika Mungu .... Habakuki 3:17-18
— Mungu ndiye asili ya furaha .... Zaburi 104:34
— Amani katika akili .... 2 Wathesalonike 3:16
— Mshukuru na umtukuze Mungu .... Zaburi 61:5,8

Mwone daktari ukiwa na sikitiko kubwa. Dawa nyingine zinaweza kusaidia wakati wa sikitiko kubwa. Soma pia katika kitabu hiki kuhusu: "Mimi sina furaha." "Mateso," na "Wasiwasi."

■ KIFO .... Tazama katika kitabu hiki: "Tumefiwa katika jamaa yetu". Pia tazama: "Shida."

■ KUKATA TAMAA Tazama "Mimi sina furaha".
Pia angalia: "Wasiwasi", na "Huzuni."

■ KUOA MKE ZAIDI YA MMOJA Kusudi la Mungu ni mtu awe na mke mmoja tu. Soma Mwanzo 2:22-24.

Mungu hutaka uaminifu kwa mke mmoja. Soma Malaki 2:14-16.

— Shida za kuwa na zaidi ya mke mmoja..Kumbukumbu la Torati 17:17
— Mfano wa ndoa iliyositawi .... Zaburi 128:1-6
— Kaeni kwa amani pale nyumbani .... Warumi 12:16-21
— Ishini kwa umoja .... Warumi 15:5-6

Tazama pia katika kitabu hiki: "Ndoa yetu ina shida". Pia angalia: "Uchungu," "Shida" na "Wasiwasi."

■ KUKOSA KAZI ...... Kukosa kazi yenye mshahara.

Uwe mvumilivu na uendelee kujaribu kutafuta kazi. Soma Yakobo 5:10-11.

Mungu atakusaidia kupata kazi. Soma Kumbukumbu la Torati 31:8.

— Omba kwa ajili ya kazi .... Yakobo 1:2-8

● Yale Mungu Anayosema Kuhusu KIFO:

Soma na ueleze juu ya vifungu hivi. Tumia Biblia yako inapowezekana. Na ikiwa haiwezekani, soma vifungu hivi kutoka katika kitabu hiki.

- Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo (Yohana 14:1-3).

- Naye atafuta kila chozi katika macho yao, wala mauti haitakuwapo tena; wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwisha kupita (Ufunuo 21:4).

- Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake (Warumi 8:28).

- Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwapo, wala wenye uwezo, wala yaliyo juu, wala yaliyo chini, wala kiumbe kinginecho chote hakitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu (Warumi 8:38-39).

- Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu. Naam nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya: kwa maana Wewe upo pamoja nami, Gongo lako na fimbo yako vyanifariji (Zaburi 23:1,4).

- Tazama, Mungu ndiye wokovu wangu; Nitatumaini wala sitaogopa: Maana Bwana Yehova ni nguvu zangu na wimbo wangu; Naye amekuwa wokovu wangu (Isaya 12:2).

Vifungu vingine ambavyo vyaweza kusomwa unapowatembelea wakati mwingine ni:

Zaburi 34:1-8	1 Wathesalonike 4:13-18
Zaburi 91:1, 14, 16	1 Yohana 4:10-21
Zaburi 116:1-15	Ufunuo 21:22-27

Pia waweza kuona katika kitabu hiki: "Shida" na "Huzuni." Angalia orodha katika ukurasa wa 5.



Waweza kusaidia watu ambao wana shida.

Anza na:

1. Kuwa na wakati wa kuwasaidia
2. Kuwa na wakati ambao wewe unaweza kupatikana.
3. Kugundua shida.
4. Kusikiliza kwa upendo wa Kikristo.

■ CHUKI ....Kuchukia, uadui, kutopenda
Heri ninyi hata wakati ule mmechukiwa. Soma Luka 6:22.

Wafanyie wema wale wanaokuchukia. Soma Luka 6:27.

- **— Yesu pia alichukiwa.. Yohana 15:18-27**
- **— Upendo ndio jibu .... Warumi 13:9**
- **— Acha upendo uendelee .... Waebrania 13:1**
- **— Chuki ni ujinga ....Tito 3:3-4**
- **— Geuza shavu lile jingine .... Mathayo 5:39**
- **— Wapende wale wanaokuchukia ....Luka 6:32-36**

Tazama: "Mimi nimekasirika sana". Pia tazama "Uchungu."

■ DHAMBI ....Uovu, makosa, hatia.
Mgeukie Bwana kwa kutubu. Soma Kumbukumbu la Torati 4:30-31.

Pokea msamaha kamili wa Mungu. Soma Waefeso 1:7.

- — Kuhuishwa na kusafishwa ....Matendo 3:19-21
- — Wema wa Mungu ....Yoeli 2:12-13
- — Pokea amani ya Mungu ....Wafilipi 4:6-7
- — Acha kutenda dhambi usijisikie kuwa mwenye hatia .Zab. 38:1-4
- — Mungu ni mwaminifu kwa kusamehe ....1 Yohana 1:8-9
- — Jisamehe mwenyewe ....Wafilipi 3:13-14

Tazama: "Nimetenda dhambi kubwa," "Mume wangu na kijana wetu si Wakristo". "Watoto wetu si Wakristo waaminifu". Pia tazama: "Shida" na "Huzuni"

■ HASIRA ....Tazama katika kitabu hiki:
"Mimi nimekasirika sana," Pia tazama: "Uchungu."

■ HATIA ....Angalia: "Nimetenda dhambi kubwa."
Pia tazama: "Shida" na "Huzuni."

■ HOFU ....Tisho, woga, kutokuwa na ushujaa.
Weka matumaini yako kwa Bwana. Soma Zaburi 56:3.

Mungu ndiye nguvu yetu.Soma Zaburi 46:1-2.

- — Amini ahadi za Mungu .... Hesabu 13:30
- — Mungu huwapa watu nguvu ....Isaya 41:10 na 12:2
- — Fanya yaliyo sawa na usiogope .... 1 Petro 3:13-14
- — Bwana ndiye msaidizi wako ....Waebrania 13:5-6
- — Upendo huondoa hofu ....1 Yohana 4:18
- — Mungu huwapa watu uwezo wa kushinda woga ...2 Timotheo 1:7

SEHEMU YA 3 — MAJIBU YA MUNGU KWA TAABU ZETU

— Msaada wa Haraka kwa Shida Zetu —

Katika kurasa zinazofuata utaona orodha ya shida mbali mbali. Mambo haya ni baadhi ya shida ambazo huwapata wanadamu mara kwa mara. Vifungu vya Biblia vimeandikwa chini ya kila jina la shida.

Hapa yaonyesha jinsi utakavyotumia sehemu hii ya kitabu hiki:

1. **Angalia shida** ambayo inakuhusu. Yaweza kuwa ni hofu, wasiwasi, uchawi, hasira au shida yo yote nyingine ambayo huwapata watu.
2. **Tazama habari fupi** iliyoandikwa upande wa kushoto ambayo itakusaidia kuchagua vifungu vya Biblia.
3. **Tafuta vifungu hivyo katika Biblia yako,** kisha umsomee yule unayemsaidia.
4. Eleza maana ya vifungu hivyo na kuvitumia kwa kusuluhisha shida ambayo unaishughulikia. **Mpe mtu unayemsaidia nafasi ya kuuliza swali** au kutoa maoni yake juu ya vifungu hivyo. Waweza kumwomba mtu huyo **kukariri na kutafakari** juu ya vifungu maalum.

Biblia ni kitabu cha Mungu - kitabu cha thamani kubwa. Biblia yatakiwa kuwa kitabu cha marejeo katika kukua kiroho.

Waweza kutumia sehemu hii ya kitabu hiki kwa njia tatu: Kwanza, unaposaidia kundi dogo la watu kutatua shida zao; pili, unapomsaidia. mtu mmoja kutatua shida yake; na tatu, ni wakati unapotayarisha mahubiri au mafundisho juu ya shida mojawapo.

Kufundisha au kuhubiri juu ya yale yaliyo katika kitabu hiki ni muhimu sana. Kwa mfano, madarasa ya vijana yaweza kuandaliwa ya kufundisha kuhusu maoni ya Kikristo juu ya: maisha, upendo, na kuhusu ndoa. Mikutano ya mafundisho ya kuimarisha ndoa inaweza kuwasaidia wale waliooana ili waweze kuimarika, kupendana na kutunza uhusiano wao wa ndoa. Mfululizo wa mahubiri juu ya yale yaliyomo katika kitabu hiki utasaidia washiriki wa kanisa lako kukua Kikristo.

Kwa hiyo, kwa kutumia orodha hii ya shida mbali mbali pamoja na vifungu vya Biblia, unaweza kupata majibu ya Mungu kwa taabu zetu.

KANUNI KUMI ZA KUWASAIDIA WATU WENGINE

Katika ukurasa wa 6 na 7 hapo nyuma ulipewa mfano wa jinsi utakavyotumia kitabu hiki. Ulisoma hatua kwa hatua jinsi unavyoweza kumsaidia mtu aliyefiwa katika jamaa yake. Pia ulipewa vifungu vya kutumia wakati unaposhauri wale walio na huzuni kwa ajili ya kifo.

Jifunze kutoka katika kitabu hiki kwa kukisoma. Tazama katika ukurasa wa 5, "Orodha ya kukusaidia kupata msaada haraka." Shida kubwa nyingi zimeandikwa pamoja na kurasa ambapo zinapatikana. Wakati shida itokeapo katika maisha ya watu ambao unaweza kuwasaidia, tafuta shida hiyo katika orodha-ukurasa wa 5. Chunguza vizuri mashauri yote, pamoja na vifungu vya Biblia. Jitayarishe kusoma vifungu vya Biblia vinavyohusiana na shida hiyo kutoka katika kitabu hiki, au usome vifungu hivyo kutoka katika Biblia yako.

Na sasa tuchunguze kanuni 10 za kuwasaidia watu wengine. Kwa kweli, usifikirie kuna suluhisho rahisi katika shida za mwanadamu. Kila mtu na kila shida ni tofauti. Ingawa hivyo, kuna mambo yenye maana ya kufanya. Hapa kuna kanuni 10 muhimu za kufuata unaposhauri watu.

1. UWE NA WAKATI WA KUWASAIDIA. Wakristo wanahitaji kuwa "watu wenye kuwajali wenzao". Watu wengi ambao wametuzunguka wana shida. Wengi wanakabiliwa na mambo yaletayo huzuni katika maisha kama talaka, ulevi, uzee na kifo. Na ni rahisi kutofanya jambo lo lote. Wewe kama kiongozi Mkristo waweza kutumia kipawa maalum ulicho nacho cha kusikiliza kwa upendo.

2. UWE NA WAKATI AMBAO WEWE UNAWEZA KUPATIKANA. Usionekane mwenye shughuli nyingi kiasi cha kutoweza kumsaidia mtu aliye na shida. Inawapasa Wakristo kujishughulisha na watu wenye shida. Kwa hivyo uwe tayari kusikiliza shida ya mtu mwingine.

3. GUNDUA SHIDA. Watu wengine watakuambia wazi juu ya shida zao. Ikiwa ni hivyo, ni vyema. Unaweza kuendelea kuwasaidia kama vile imeelezwa katika kitabu hiki. Ikiwa unafikiria kuna shida, na mtu anasitasita kukueleza, unaweza kufanya nini? Katika hali hiyo unaweza kusema, "Watu wengi siku hizi wana shida ya hofu, huzuni, hasira, umaskini na kadhalika. Niko tayari kukusaidia ikiwa una shida yo yote. Je, una shida ambayo ungetaka kuniambia ili nione kama ninaweza kukusaidia?"

4. SIKILIZA KWA UPENDO WA KIKRISTO. Hii inaonyesha kujali kama jinsi Mungu anavyomjali mtu aliye na shida. Ina maana kwamba

usikilize kwa makini ili uweze kukusanya mambo yote muhimu kuhusu tatizo hilo. Kusikiliza kwa upendo wa Kikristo ni kusikiliza kwa uangalifu ili baadaye SULUHISHO lipatikane. Ni muhimu kujua kabisa haja halisi ya mtu unayemsaidia. Kwa hivyo tega sikio usikie yale yote yanayosemwa. Wakati mtu mwingine anapozungumza, usiwe ukifikiria jibu ambalo utalitoa, bali badala ya kufanya hivyo, endelea kusikiliza. Kwa kawaida majibu ya haraka hayasaidii. Kwanza, tumia wakati mwingi kwa kusikiliza kuliko kuzungumza. Sikiliza jinsi ambavyo ungetaka watu wengine wakusikilize.

Hapa kuna mfano wa kanuni nne za kwanza: Mchungaji Timotheo alisikia juu ya mwanamke katika kijiji chao ambaye alikufa. Alitumia wakati wake kwenda kuwafariji wale waliofiwa. Baada ya kumsalimia mume wa mke ambaye alikufa, Mchungaji Timotheo alisema: "Nilisikia habari za kuhuzunisha juu ya kifo cha mke wake."

Mume: "Ndiyo, hii ilitokea jana."

Mchungaji: "Bila shaka huu ni wakati wa huzuni kwenu. Niliposikia juu ya mke wako, nilikumbuka kifo cha mtoto wangu aliyekufa miaka miwili iliyopita. Ulikuwa wakati wa huzuni kwetu sisi sote. Je, ndugu, unaweza kuniambia zaidi juu ya msiba huu wa mke wake."

Mume: (Hapo mume anasema kwa dakika chache juu ya mke wake, ugonjwa wake na kifo chake.)

Mchungaji: (Baada ya kusikiliza bila kusema cho chote, baadaye anasema,) "Kwa kweli ninajua umeshtushwa na kifo cha mke wako na watoto wako wanasikiaje kuhusu kifo cha mama yao?

Mchungaji Timotheo alimsaidia mume wa mama aliyekufa kwa sababu alitumia wakati wake kumsaidia na hata kwenda nyumbani kwa yule aliyefiwa. Alisikiliza kwa upendo wa Kikristo naye akaelewa juu ya shida hiyo. Baadaye Mchungaji Timotheo aliendelea kusaidia akitumia hatua zifuatazo.

5. ULIZA MASWALI KWA BUSARA. Ili kumsaidia mtu katika shida yake, ni lazima ujue MAMBO YALIYO MUHIMU kuhusu taabu yake. Pia inakupasa ujaribu kuelewa jinsi ANAVYOJISIKIA kuhusu mambo yanayosababisha shida yake. Kwa hivyo sikiliza kwa uangalifu majibu kamili ya maswali kama haya yafuatayo:

A) Je, unafikiria **shida** hiyo hasa ni nini?

B) **Unasikiaje** juu ya shida hiyo?

Yale Biblia Inayosema Kuhusu KUKUA KATIKA MAISHA YA KIKRISTO:

Ukipata wakati na nafasi nzuri, wasomee na kuwaeleza watoto wako vifungu hivi:

- (Mungu akasema) Kwa hiyo yawekeni maneno yangu mioyoni mwenu na rohoni mwenu; yafungeni yawe dalili juu ya mikono yenu, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yenu. Nayo wafunzeni vijana wenu kwa kuyazungumza uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo na uondokapo (Kumbukumbu la Torati 11:18-19).
- Nanyi, akina baba, msiwachokoze watoto wenu, bali waleeni katika adabu na maonyo ya Bwana (Waefeso 6:4).
- Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wokovu (1 Petro 2:2).
- Yeye aliye na amri zangu na kuzishika, yeye ndiye anipendaye (Yohana 14:21).
- Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele (Yohana 10:10).
- Ombeni, nanyi mtapata, furaha yenu iwe timilifu (Yohana 16:24).
- Hamjui ya kwamba kuwa rafiki wa dunia hujifanya kuwa adui wa Mungu (Yakobo 4:4).
- Mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu (Mathayo 4:4).
- Tukaangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja (Waebrania 10:24-25).
- Ufanye bidii katika kusoma na kuonya na kufundisha (1 Timotheo 4:13).
- Jitahidi kujionyesha kuwa umekubaliwa na Mungu, mtenda kazi asiye na sababu ya kutahayari (2 Timotheo 2:15).

Washauri watoto wako wajiunge na Masomo ya Biblia kwa Njia ya Posta (Bible Correspondence Course). Angalia pia katika kitabu hiki: "Mkristo kurudi nyuma," "Dhambi," na "Shida za Jamaa." Tazama orodha katika ukurasa wa 5.

"WATOTO WETU SI WAKRISTO WAAMINIFU."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Wasikilize kwa upendo wazazi ambao wanahuzunika juu ya jinsi watoto wao wanavyoishi.
2. Ikiwa watoto hawaishi pale nyumbani pamoja na wazazi wao, jambo bora zaidi la kufanya ni kuendelea kuwaombea wale ambao ni wakubwa. Pia, washauri kwamba wakati upangwe wa kukutana na watoto hao walio wakubwa. Kisha, kwa uvumilivu na upole, wazazi wanaweza kushirikiana na watoto wao mambo yale ambayo Mungu anawafundisha kutoka katika Biblia. (Tazama vifungu vya Biblia katika ukurasa unaofuata.)
3. Ikiwa watoto wangali wanaishi nyumbani pamoja na wazazi, washauri mambo yafuatayo:
   A. Tumia wakati mwingi pamoja na watoto wako na kujua mahitaji na shida zao.
   B. Tafuta nafasi kila siku ili kuonyesha upendo wa Mungu na upendo wako kwa watoto wako.
   C. Kuwa na tabia kamili ya kuhudhuria kanisa, kusoma Biblia na kuomba pamoja na watoto.
   D. Kuwa karibu na watoto wako ili uweze kuwaleta kwa Yesu.
   E. Ondoa vizuizi katika jamaa yako ambavyo vyaweza kuzuia hali ya kukua Kikristo.
   F. Sitawisha uvumilivu na uaminifu.
   G. Hakikisha kwamba watoto wako wamemkubali Yesu Kristo kama Bwana na Mwokozi wao. Ikiwa mmoja wao si Mkristo, tumia mpango ule ulioonyeshwa katika kitabu hiki chini ya kichwa "Mume wangu na kijana wetu si Wakristo," ukurasa wa 36 na 37.
4. Omba upate nafasi ya kushirikiana pamoja katika Neno la Mungu kama inavyoonyeshwa katika ukurasa unaofuata.

C) **Umefanya nini** kuhusu taabu hiyo?

D) **Je, unafikiria ni nini unachoweza kufanya zaidi** ya yale ambayo umefanya?

E) Unafikiri **Mungu** anataka jambo gani lifanywe kuhusu shida hiyo?

6. ELEZA SHIDA HIYO KWA NJIA NYINGINE. Eleza tatizo hilo kwa kifupi jinsi unavyoielewa sasa. Tumia baadhi ya maneno yaliyotumiwa na yule mwenye shida. Ufupisho huo wa yale uliyoyasikia unakusaidia kufahamu vizuri zaidi bila makosa juu ya mambo muhimu katika taabu hiyo. Pia jambo hilo linakusaidia kuepuka kujaribu kutatua shida ambayo huielewi. Sasa umelichunguza tatizo lenyewe, ukajua kilichosababisha shida hiyo, na jinsi mtu huyo anavyojisikia kutokana na taabu hiyo.

7. ANZA KUSAHIHISHA FIKIRA ZISIZO SAHIHI. Eleza ya kwamba shida nyingi maishani zinaletwa na FIKIRA ZISIZO SAHIHI. Mara nyingi shida yenyewe sio yale hasa yanayotupata, bali ni vile tunavyofikiria na kuwaza juu yetu sisi wenyewe tukiwa katika hali hiyo ya shida. Mawazo mabaya ndiyo kiini cha shida nyingi. Kwa hiyo msaidie mtu ambaye ana shida kuwa na mawazo mema badala ya mawazo mabaya au maovu.

Kwa mfano Bi. Matheu alijisikia mwenye uzito moyoni na huzuni nyingi. Naye akaenda kuzungumza na mke wa Mchungaji Timotheo aitwaye Grace.

Bi. Matheu: "Mimi ni mjinga. Sina jambo ninalofanya vizuri. Je, mimi ni ovyo namna gani?"

Grace: "Ngoja sasa, tafadhali uniambie yaliyotokea."

Bi. Matheu: (Anachukua kama dakika kumi kueleza shida yake, na kumjibu Grace maswali yake.)

Grace: "Hebu nijaribu kukuambia yale uliyonieleza kwa kifupi." (Baada ya kueleza kwa kifupi, Grace anaendelea:) "Sasa, tujaribu kusahihisha mawazo uliyo nayo kuhusu wewe mwenyewe. Sioni kama wewe ni mjinga hata kidogo, kama ulivyosema. Hufanyi mambo yote vibaya, kwa hiyo na tuchunguze baadhi ya mambo yasiyo sahihi unayofikiria juu yako mwenyewe."

8. SISITIZA JUU YA KUTAFUTA SULUHISHO. Makusudi mawili muhimu ya kuzungumza juu ya shida ni: 1) Kutumika katika maendeleo

ya kibinadamu katika maisha ya Kikristo. 2) Kuwasaidia watu kutafuta suluhisho katika shida zao. **Msimamo wa kitabu hiki ni kwamba watu walio na shida wanahitaji SULUHISHO.** Kwa kweli, si kupeana mashauri ya haraka au majibu rahisi kwa kila shida. Lakini lengo kubwa kwako na kwa yule mwenye shida ni kupata SULUHISHO. Suluhisho huleta mabadiliko katika mawazo na katika matendo.

9. TUMIA MAANDIKO YALIYOCHAGULIWA. Kutumia Neno la Mungu ipasavyo huelekeza watu katika suluhisho la kweli. Usisome tu kutoka katika Biblia kabla hujamsikiliza mtu mwenye shida. Kumbuka hatua nane ambazo tumejifunza sasa. Sasa wewe uko tayari kuanza kutumia maandiko yaliyochaguliwa kama yalivyotolewa katika kitabu hiki. Neno la Mungu ni neno lenye nguvu. Mungu ana uwezo **wa** kumkomboa yule anayetaabika, na kumfanya awe huru. **KITABU HIKI KIMETAYARISHWA ILI KIKUSAIDIE KUTUMIA BIBLIA KWA UANGALIFU, KWA IMANI NA KWA NJIA ILIYO SAHIHI.** Baada ya kusoma na kueleza vifungu kadhaa, omba ili Roho wa Mungu amsaidie yule mtu apate suluhisho la shida yake.

10. PANGA WAKATI WA KUKUTANA TENA. Inaweza kuwa vyema kukutana na mtu unayemsaidia au jamaa nzima baada ya juma moja kwa mazungumzo zaidi. Mhakikishie mtu yule ya kwamba **utaendelea kuomba ili Mungu aendelee kufanya kazi katika maisha yake na kumsaidia kutatua shida yake.**

● Yale Biblia Inayosema Kuhusu WOKOVU:

Msomee na umweleze mtu anayehitaji wokovu vifungu vinavyofuata. Tafuta vifungu hivi kutoka katika Biblia yako.

1. **Mungu ametupa uhai na baraka nyingi.**

   Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba (Mwanzo 1:27).

   Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka juu, hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka (Yakobo 1:17).

2. **Kipawa cha Mungu cha thamani kubwa zaidi kwetu ni mwanawe Yesu.**

   Mungu, ambaye alisema zamani na baba zetu katika manabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana (Waebrania 1:1-2).

   Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16).

3. **Unaweza kupokea kipawa cha Mungu sasa kwa kutubu na kumwamini Yesu.**

   Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:9).

   Mwamini Bwana Yesu, nawe utaokoka pamoja na nyumba yako (Matendo 16:31).

Baada ya kufanya hayo yaliyo juu, ingekuwa vyema kuomba maombi mafupi ya kumpokea Yesu, kama hivi: "Yesu, Unisamehe dhambi zangu zote. Ninakupokea kwa imani. Ninakushukuru kwa kuingia katika maisha yangu. Amina." Au umwache aombe mwenyewe vile anavyotaka.

Baada ya maombi sema hivi: "Kwa kuwa sasa wewe ni Mkristo mpya, itakuwa vyema usome Biblia, kuomba na kuwa mshiriki wa kanisa." Endelea kumsaidia Mkristo huyo mpya katika kila jambo, na kujibu maswali yo yote yatokeapo.

"MUME WANGU NA KIJANA WETU SI WAKRISTO."

1. Kubali ya kwamba mke Mkristo ana wajibu mkubwa katika wokovu wa jamaa yake.
2. Hata hivyo, onyesha wazi ya kwamba mke Mkristo anastahili kumheshimu mumewe ingawa yeye si Mkristo. Mke huyo anatakiwa pia awe mvumilivu katika ushuhuda wake. Jambo muhimu katika kumleta mumewe au mwanawe kwa Kristo ni kuonyesha upendo na uvumilivu wa Kikristo.
3. Eleza ya kwamba maisha ya Kikristo na kusema ushuhuda wa Kristo ni mambo muhimu. Maisha mazuri yenye upole na unyenyekevu pamoja na ushuhuda wa kusema vyaweza kuwaleta jamaa kwa imani katika Kristo.
4. Eleza ya kwamba kujua la kusema na jinsi ya kulisema ni mambo ambayo mtu anaweza kujifunza. Tazama mpango wa kushuhudia hatua kwa hatua katika ukurasa unaofuata. (Yampasa Mchungaji kuandaa mafunzo ya muda mfupi kuhusu "Jinsi ya kumshuhudia Kristo.")
5. Njia nyingine ya kushuhudia ni kama ifuatayo. Mke anaweza kutumia mfano wa mawe matatu yanayotumiwa jikoni. Mawe yote matatu yanahitajika katika kushikilia sufuria pale jikoni. Vivyo hivyo, kuna mambo matatu muhimu katika kuwa Mkristo: Yesu, Biblia na kanisa. Basi, mke anaweza kuzungumza juu ya mambo hayo matatu katika maisha yake.
6. Mshauri mke kukumbuka yafuatayo:
   - A. Anaweza kuzungumza juu ya uwezo wa Kristo shida itokeapo, kama: ugonjwa, habari mbaya, kifo, n.k.
   - B. Kuna wakati wa kuzungumza juu ya Kristo na kuna wakati wa kuwa kimya.
   - C. Anaweza kuzungumza na Mungu moyoni katika maombi kuhusu jamaa yake.
7. Tumia wakati wako na ushuhuda kutafuta njia ya kuwaleta mume na kijana wake kwa Yesu.

MAMBO USIYOSTAHILI KUYAFANYA

1. Usizungumze juu ya shida pekee; zungumza pia juu ya SULUHISHO KUTOKA KWA MUNGU. Sisitiza juu ya KUMTII MUNGU, ingawa mtu huyo anajisikia hataki.
2. Usikose kuzungumza juu ya umuhimu wa MATUMAINI. Katika Neno la Mungu na Roho wa Mungu, daima kuna matumaini kwa watu wa Mungu.
3. Usizungumze na kuonekana mwenye majibu yote. Waongoze watu wanapoendelea kukata shauri yao wenyewe.
4. Usipeleleze siri ambazo hajakufunulia.
5. Usikose kuwa na lengo la MABADILIKO katika mawazo na tabia.
6. Usijaribu kubadilisha yale ambayo hayawezi kubadilishwa. Jifunze kukubali na kuwaongoza wengine ili wakubali.
7. Usikose kutambua maneno na mawazo muhimu. Kuwa mtulivu na mwenye moyo wa kutaka kusaidia.
8. Usijaribu kushinda katika mabishano au kutoa mashauri kwa kila jambo. Upendo na huruma yako ni vya maana zaidi kuliko shauri lo lote ambalo ungelitoa.
9. Ukiwa mwanamume, usikubali kumshauri mwanamke ukiwa peke yako.
10. Usikose kutoa ushuhuda wako kama Mkristo. Lengo lako liwe kuwaleta wasio Wakristo na shida zao kwa Kristo kama Mwokozi na Bwana. Tazama katika kitabu hiki: "Mume wangu na kijana wetu sio Wakristo," tazama ukurasa wa 36.
11. Usimwambie mtu mwingine juu ya shida zile ambazo mmezungumza juu yake. Yale ambayo umeambiwa kwa siri, lazima yawe siri.
12. Usife moyo ikiwa huwezi kumsaidia kila mtu.
13. Usikose kutumia yale ambayo umeyapata kutoka katika kitabu hiki katika mahubiri na mafundisho yako.
14. Usikose kutambua umuhimu wa madarasa au mikutano ya makundi madogo madogo kulishauri kanisa lako juu ya suluhisho la Biblia kuhusu shida.
15. Usisahau kutayarisha moyo wako kila siku kwa njia ya maombi.

SEHEMU YA 2 - KUWASAIDIA WENYE SHIDA

Hapa kuna njia za kuwasaidia watu walio na shida.

"MIMI NIMEKASIRIKA SANA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Msaidie mtu aliyekasirika kuelewa hasira yake. Pengine amekasirishwa na yale ambayo mtu mwingine amemwambia au kumtendea.
2. Mweleze yule aliyekasirika ya kwamba hasira inaweza kuondoa furaha yake. Hasira ni kama moto mkubwa, tena ni kama sumu.
3. Mwambie ya kwamba hasira huletwa na: A) kuishi maisha yasiyo huru; B) kutaka kitu kwa nguvu zako zote na baadaye ukikose; C) kuumia mawazo; au D) hofu yetu na kiburi chetu.
4. Sasa soma pamoja na yule mwenye hasira vifungu vya Biblia katika ukurasa unaofuata. Baada ya kusoma vifungu hivyo, endelea na mashauri yaliyomo katika ukurasa huu. Ugomvi na mabishano vyahitaji kusuluhishwa mara moja.
5. Mwambie ya kwamba Mungu anaweza kumpatia suluhisho kwa shida ambazo zilimfanya akasirike. Kuvumilia hasira ndani yako si vizuri, bali badala yake yapasa hasira kuchukuliwa kwa njia inayompendeza Mungu.
6. Eleza wazi ya kwamba mapenzi ya Mungu ni KUMSAMEHE YULE MTU MWINGINE. Hii ndiyo amri ya Yesu. Ni lazima tusameheane kwa sababu twampenda Yesu. Tusameheane kwa sababu tumesamehewa na Mungu. Tusameheane mara nyingi jinsi Mungu anavyotusamehe.
7. **Mshauri yule mwenye hasira aende haraka kwa yule ambaye amemkasirisha. Yawapasa watu hao wawili wasameheane. Katika kufanya hivi, ataweza kuwa na uhusiano mwema na ndugu au dada yake.**

Jinsi Neno la Mungu Linavyosema Kuhusu UCHAWI na PEPO WACHAFU:

Tumia vifungu hivi, ukieleza maana yake:

- Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani (Mathayo 28:18).
- Kwa sababu hiyo nawaambia, yo yote myaombayo mkisali, aminini ya kwamba mnayapokea, nayo yatakuwa yenu (Marko 11:24).
- Basi mtiini Mungu. Mpingeni Shetani, naye atawakimbia (Yakobo 4:7).
- Kwa sababu yeye aliye ndani yenu (Roho wa Mungu) ni mkuu kuliko yeye aliye katika dunia (1 Yohana 4:4).
- Nguvu zina Mungu (Zaburi 62:11).
- Yeye (Mungu) huwapa watu wake nguvu na uwezo (Zaburi 68:35).
- Yesu akamkemea, akisema, fumba kinywa, umtoke. Yule pepo mchafu akamtia kifafa, akalia kwa sauti kuu, akamtoka (Marko 1:25-26).
- Pepo nao waliwatoka watu wengi, wakipiga kelele na kusema, "Wewe u Mwana wa Mungu" (Luka 4:41).
- Ndipo wale sabini waliporudi kwa furaha wakisema, "Bwana, hata pepo wanatutii kwa jina lako" (Luka 10:17).
- "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga" (Yohana 14:27).
- Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na moyo wa kiasi (2 Timotheo 1:7).

Soma vifungu hivi pia:

Zaburi 54:1-7	Waefeso 6:10-18
2 Wakorintho 4:7-10	Wafilipi 4:6-7
Wagalatia 5:1	Waebrania 13:6

Tazama pia katika kitabu hiki kuhusu: "Hofu", "Shetani" na "Ugonjwa," katika orodha, ukurasa wa 5.

"KIJANA WETU ANAZUNGUMZA UPUZI — JE, AMEROGWA?"

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Kubali ya kwamba uchawi husababisha hofu kuu. Inaaminika ya kwamba wachawi husababisha shida za aina nyingi: ugonjwa usiopona haraka, ugonjwa wa akili, utasa, kuzaliwa na kilema, na kifo cha mifugo na watu. Cho chote ambacho kinaaminiwa kuwa ni cha kweli kinapaswa kichukuliwe kuwa ni cha kweli.
2. Wasikilize kwa huruma wale watu wanaosumbuliwa na uchawi. Hata Wakristo wanaweza kuamini ya kwamba watu wengine wanaweza kuwadhuru kwa uchawi.
3. Waambie wazazi wa kijana anayezungumza mambo ya upuzi ya kwamba Ukristo unasuluhisha shida nyingi. Mambo matatu yanaweza kuangaliwa: 1) Wasihi Wakristo kumwombea kijana huyo sana, 2) Wampeleke kwa daktari halisi, 3) Kijana aletwe kwako ili kupata msaada.
4. Kijana huyo akija kwako, fanya kama ifuatavyo:
   A. Ikiwa atazungumza, sikiliza juu ya shida yake. Jaribu kujua kama yeye ni Mkristo wa kweli.
   B. Mwambie juu ya uwezo wa Mungu juu ya Shetani.
   C. Soma na kueleza vifungu vya Biblia katika ukurasa unaofuata.
   D. Mwombe Mungu akupe nguvu za kumshinda Shetani. Omba ya kwamba nguvu za Kristo zitaleta ushindi kamili.
   E. Endelea kumwomba Mungu ukimshukuru kwa ajili ya ushindi.
5. Endelea kutoa msaada kwa kijana huyo na wazazi wake. Mtu ambaye ameondokewa na hofu ya uchawi anahitaji kujazwa na Roho wa Mungu, uweza wa Mungu, na Neno la Mungu. Onyesha jamaa jinsi ambavyo hayo yanaweza kufanyika.
6. Panga tarehe na mahali ambapo mtakutana na kuzungumza na watu hao tena.

Yale Mungu Anayosema Kuhusu HASIRA:

Tumia vifungu hivi mnapotoa mashauri juu ya hasira. Msomee na umweleze aliye na hasira vifungu hivi.

- Usifanye haraka kukasirika rohoni mwako, maana hasira hukaa kifuani mwa wapumbavu (Mhubiri 7:9).
- Jawabu la upole hugeuza hasira; bali neno liumizalo huchochea ghadhabu (Mithali 15:1).
- Asiye mwepezi wa hasira ni mwema kuliko shujaa; Na mtu aitawalaye roho yake kuliko mtu atekaye mji (Mithali 16:32).
- Mmesikia watu wa kale walivyoambiwa, usiue; na mtu akiua, itampasa hukumu. Bali mimi nawaambieni, kila amwoneaye ndugu yake hasira itampasa hukumu; na mtu akimfyolea ndugu yake, itampasa baraza; na mtu akimwapiza, itampasa jehanum ya moto (Mathayo 5:21-22).
- Amri mpya nawapa, mpendane. Kama vile nilivyowapenda ninyi, nanyi mpendane, vivyo hivyo. Hivyo watu wote watatambua ya kuwa ninyi mmekuwa wanafunzi wangu, mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi (Yohana 13:34-35).
- Hayo mnajua, ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika (Yakobo 1:19).
- Ee Mungu, uniumbie moyo safi, uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu (Zaburi 51:10).

Vifungu vingine vya kusoma ni:

Mathayo 5:38-41	Mathayo 18:21-22
Mathayo 5:43-44	1 Wathesalonike 5:15
Mathayo 6:14-15	1 Yohana 4:7-8

Tazama pia katika kitabu hiki kuhusu: "Uchungu" na "Shida". Angalia orodha katika ukurasa wa 5.

"MIMI NI MGONJWA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Mpe yule aliye mgonjwa moyo, matumaini na furaha. Anahitaji nguvu ambazo huletwa na imani na tumaini. Labda hawezi kuendelea kuvumilia maumivu na hofu yake. Kwa hiyo, mwambie habari za upendo wa Mungu na uwezo wake wa kuponya.
2. Msaidie mgonjwa kuona ya kwamba ugonjwa unaweza kuleta jambo la msaada. Mungu anaweza kutumia ugonjwa kumfundisha mtu uvumilivu au kumfundisha shukrani kwa ajili ya afya.
3. Kama msaada wa hospitali unahitajika, hakikisha kwamba umepatikana. Madaktari na dawa nzuri zimeweza kurejesha afya kwa wagonjwa wengi. Elimu ambayo madaktari wanayo ni kipawa kutoka kwa Mungu. Kutumia madawa ni kutumia baadhi ya vipawa ambavyo Mungu ametupatia.
4. Wakumbushe watu wote ya kwamba haiwapasi Wakristo kwenda kwa wachawi. Hilo ni jaribu kubwa kwa watu wengine. Mungu ana uwezo wote. Kwa hiyo, ni dhambi kugeukia uchawi.
5. Wapatie walio wagonjwa wakati wa kutubu dhambi zao. Wengine ambao ni wagonjwa wana uchungu juu ya Mungu. Wengine wana tabia ya kunung'unika na wengine wana dhambi ambazo hawajatubu. Mara nyingi kutubu dhambi husaidia katika kuponya magonjwa.
6. Msaidie mgonjwa, ikiwa yeye hajaokolewa, amwamini Yesu kama Bwana na Mwokozi wake.
7. Mwombee huyo aliye mgonjwa. Maombi yako yapasa kuonyesha imani kwa Mungu na kuwa mwongozo kwa yule aliye mgonjwa. Maombi yako yaambatane na mahitaji yao, kwa sababu kuna nguvu katika maombi.
8. Omba uwezo kutoka kwa Mungu kwa kusoma Biblia. Mwachie mgonjwa kijikaratasi cha Neno la Mungu au orodha ya vifungu vya Biblia, ili awe akisoma kila siku nyumbani.
9. Hakikisha ya kwamba wazee au baadhi ya wanawake wa kanisa wanajua mahitaji ya yule mgonjwa. Yawapasa Wakristo kuwahudumia walio wagonjwa,

Yale Mungu Anayowaambia Wale Wanaotaka KUOANA:

Wasomee na kuwaeleza vifungu hivi watu wanaopanga kuoana:

- Bwana Mungu akasema, si vyema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye (Mwanzo 2:18).
- Apataye mke apata kitu chema; naye ajipatia kibali kwa Bwana (Mithali 18:22).
- Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu; na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe (1 Petro 3:7).
- Enyi wake, watiini waume zenu kama kumtii Bwana wetu. Kwa maana mume ni kichwa cha mkewe, kama Kristo naye ni kichwa cha kanisa; naye ni mwokozi wa mwili. Enyi waume, wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda kanisa, akajitoa kwa ajili yake (Waefeso 5:22-23, 25).
- Mke mwema, ni nani awezaye kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani. Moyo wa mumewe humwamini, wala hatakosa kupata mapato. Humtendea mema wala si mabaya, siku zote za maisha yake. Nguvu na hadhi ndiyo mavazi yake; Anaucheka wakati ujao. Hufumbua kinywa chake kwa hekima, na sheria ya wema i katika ulimi wake (Mithali 31:10-12, 25-26).
- Usinisihi nikuache, Nirejee nisifuatane nawe; maana wewe uendako nitakwenda, na wewe ukaapo nitakaa. Watu wako watakuwa watu wangu, Na Mungu wako atakuwa Mungu wangu (Ruthu 1:16).
- Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote (1 Wakorintho 13:4-7).

Tazama pia katika kitabu hiki kuhusu: "Watoto," "Uasherati:" "Ngono," "Kuoa mke zaidi ya mmoja," na "Wasiwasi." Tazama orodha katika ukurasa wa 5.

"TWATAKA KUOANA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Anza kwa kuwaambia wale watakao kuoana ya kwamba mtazungumza juu ya sherehe za arusi baadaye. Wajibu wako wa kwanza ni kuwashauri hao wawili juu ya kanuni za ndoa ya Kikristo.
2. Uliza kwa makini, ili upate kujua kama hao wawili wako tayari na wanastahili kuingia katika ndoa. Kunaweza kuwa na shida kama wazazi kukataa, talaka ambazo hazikusuluhishwa, tofauti za dini au madhehebu, umri wao na kadhalika. Kwa hivyo, ikiwa shida kama hizo haziwezi kusuluhishwa, pengine hutakiwi kuwaoza hao wawili.
3. Shauriana na hao wawili mambo yafuatayo:
   - A. Ndoa ipo katika mpango wa Mungu.
   - B. Njia za kuleta furaha katika ndoa.
   - C. Njia za kutatua shida katika ndoa.
   - D. Ndoa yenye msingi wa upendo wa Kikristo.
   - E. Ngono katika ndoa.
   - F. Wajibu wa wazazi juu ya watoto.
   - G. Matumizi ya posa katika ndoa.
   - H. Mpango wa wakati wa maombi ya jamaa nzima nyumbani.
   - I. Umuhimu wa kuendelea kuwa washiriki imara kanisani.

   (Ikiwa wewe kama kiongozi wa kanisa unahitaji msaada wo wote kuhusu mambo yaliyo hapo juu, nunua na usome kitabu kiitwacho: "*Maisha ya Jamaa ya Kikristo.*" Andika kwa: Evangel Press, Box 28963, Nairobi, Kenya.)
4. Waombee wanaotaka kuoana wasome kijitabu kidogo kuhusu maisha ya jamaa ya Kikristo. (Kwa mfano, wapatie kile kinachoitwa, "*Maisha ya Kila Siku.*" Chapatikana bure katika lugha ya Kiingereza, Kifaransa na baadhi ya lugha nyingine za hapa Afrika. Andika kwa: Scripture Gift Mission, Eccleston Street, London SW1W 9LZ).
5. Panga wakati mwingine wa kuweza kuzungumza na hao wanaotaka kuoana kuhusu mambo yaliyosalia kutokana na yale mliyoyazungumza hapo juu. Wakati huo wewe pamoja na hao wawili mwaweza kufanya mipango juu ya harusi.

Yale Neno la Mungu Linayofundisha Kuhusu UGONJWA NA MAUMIVU:

Msomee na umweleze mtu aliye mgonjwa vifungu hivi vya Biblia:

- Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu (2 Wakorintho 1:3-4).
- Naye akaniambia, neema yangu yakutosha; maana uweza wangu hutimilika katika udhaifu (2 Wakorintho 12:9a).
- Kwa maana nayahesabu mateso ya wakati huu wa sasa kuwa si kitu kama utukufu ule utakaofunuliwa kwetu (Warumi 8:18).
- Ee Bwana, Mungu wangu, nalikulilia ukaniponya (Zaburi 30:2).
- Na jua lilipokuwa likichwa, wote waliokuwa na wagonjwa wenye maradhi mbali mbali waliwaleta kwake, akaweka mikono yake juu ya kila mmoja, akawaponya (Luka 4:40).
- Huwapa nguvu wazimiao, humwongezea nguvu yeye asiyekuwa na uwezo (Isaya 40:29).
- Uniponye, Ee Bwana, nami nitaponyeka; uniokoe, nami nitaokoka; kwa maana wewe ndiwe uliye sifa zangu (Yeremia 17:14).
- (Yesu akasema) "Mimi nalikuja ili wawe na uzima, kisha wawe nao tele (Yohana 10:10).

Vifungu vingine vya kusoma ni:

Zaburi 32:1-4
Zaburi 38:15-18
Zaburi 119:67,71
Isaya 40:31
2 Wakorintho 1:6-7

Tazama pia: "Wasiwasi," "Huzuni" na "Hofu" katika orodha, ukurasa wa 5.

"MIMI SINA FURAHA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Msikilize kwa makini mtu aliye na shida. Mtu asiye na furaha hujisikia kuwa na upweke, mwenye huzuni na pia huwa anaona kama mambo yote hayafai. Onyesha upendo wako kwa kuwepo pamoja naye anapokuhitaji.
2. Zungumza na huyo asiye na furaha juu ya matumaini mema. Biblia ina suluhisho kwa shida zetu. Yesu ndiye jibu, tena kuna tumaini kwa kila shida.
3. Mshauri yule ambaye hana furaha kuendelea na kazi zake. Kusimamisha kazi yake kunaweza kufanya shida yenyewe kuwa mbaya zaidi.
4. Msaidie kuwafikiria na pia kuwatendea watu wengine. Watu wasio na furaha hutumia wakati mwingi wakifikiria juu ya shida zao wenyewe.
5. Mshauri ya kwamba kutokuwa na furaha kunaweza kutokana na dhambi. Kutokuwa na furaha ni ishara ya kwamba jambo fulani haliko sawasawa. Labda asiye na furaha anahitaji kutubu na kuungama dhambi iliyojificha moyoni mwake. Anaweza kuwa amejikasirikia mwenyewe, au kuwakasirikia watu wengine, au Mungu pia.
6. Someni pamoja vifungu kutoka katika Biblia. Katika ukurasa ufuatao vifungu vya Biblia vimetolewa juu ya "furaha".
7. Mwombe akuambie ni mambo gani ambayo humfanya awe na furaha. Pengine anahitaji wakati kufikiria jambo hili. Mwombe akuambie jambo lo lote lililomfurahisha.
8. Omba pamoja naye ikiwezekana. Omba maombi ya shukrani kwa ajili ya upendo wa Mungu unaosamehe dhambi zote. Mshukuru Mungu kwa ajili ya uwezo wake unaoweza kusuluhisha shida zote.
9. Panga wakati wa kukutana na mtu huyo tena hivi karibuni.

Msaada Kutoka Katika Biblia Kuhusu ULEVI:

Eleza kwa makini vifungu hivi vya Biblia wakati unapowasaidia walio na shida ya ulevi.

- Msidanganyike; Mazungumzo mabaya huharibu tabia njema. Tumieni akili kama ipasavyo, wala msitende dhambi, kwa maana wengine hawamjui Mungu. Ninanena hayo niwafedheheshe (1 Wakorintho 15:33-34).
- Tena msilewe kwa mvinyo, ambamo mna ufisadi; bali mjazwe Roho (Waefeso 5:18).
- Ni nani apigaye, Yowe? Ni nani aliaye, Ole? Ni nani mwenye ugomvi? Ni nani mwenye mguno? Ni nani aliye na jeraha zisizo na sababu? Ni nani aliye na macho mekundu? Ni wale wakaao sana kwenye mvinyo; Waendao kutafuta divai iliyochanganyika (Mithali 23:29-30).
- Mvinyo hudhihaki, kileo huleta ugomvi; na akosaye kwa vitu hivyo hana hekima (Mithali 20:1).
- Umtwike Bwana mzigo wako naye atakutegemeza, Hatamwacha mwenye haki aondoshwe milele (Zaburi 55:22).
- Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yalio ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo (Wafilipi 4:8).
- Ni huruma za Bwana kwamba hatuangamii, kwa kuwa rehema zake hazikomi. Ni mpya kila siku asubuhi: Uaminifu wako ni mkuu. Bwana ndiye fungu langu, husema nafsi yangu, kwa hiyo nitamtumaini yeye, Bwana ni mwema kwa hao wamngojeao, kwa hiyo nafsi imtafutayo (Maombolezo 3:22-25).
- Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote, na katika mambo yo yote, tumefundishwa kushiba na kuona njaa, kuwa na vingi na kupungukiwa. Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu (Wafilipi 4:12-13).

Tazama pia katika kitabu hiki: "Nina tamaa kubwa zisizo za Kikristo," "Mume wangu na kijana wetu si Wakristo," na "Nimetenda dhambi kubwa." Pia tafuta: "Wasiwasi," "Shida," na "Huzuni," katika orodha, ukurasa wa 5.

"MUME WANGU HUNYWA POMBE SANA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Inaonekana ya kwamba hakuna matumaini katika shida yake. Ulevi ni mazoea ambayo yameleta uharibifu mkubwa katika maisha ya watu milioni nyingi. Ingawa hivyo, kuna matumaini.
2. Chukua hatua moja moja hadi mwishowe shida yenyewe itakapokomeshwa. Eleza umuhimu wa kuishi leo bila kuwa na wasiwasi kuhusu kesho.
3. Eleza jinsi ulevi wa kupindukia unavyotokea: kwa ajili ya marafiki wanaolewa, maisha ya nyumbani yasiyo na furaha, hofu kutofaulu katika maisha na kuingiwa na ulevi.
4. Mlevi huvutwa na fadhili na uthabiti kuliko lawama na vitisho. Kulaumu kosa ni bure. Anahitaji uongozi ili aweze kushinda ulevi.
5. Panga jinsi utakavyozungumza na yule mlevi wewe mwenyewe. Msaidie aelewe na kukubali ya kwamba shida ya ulevi aliyo nayo ni mbaya sana. Msaidie aone matokeo mabaya yanayoweza kutokea katika afya yake na katika jamaa yake ikiwa ataendelea na ulevi.
6. Mweleze mlevi juu ya uweza wa Mungu. Injili ya Kristo imewaokoa maelfu ya walevi – hata wakati ambao njia nyingine zote zimeshindwa.
7. Jaribu kumwongoza mlevi apate wokovu kamili katika Kristo. Tazama ukurasa wa 36 na 37 kwa mashauri zaidi. Kumgeukia Kristo kwaweza kuleta furaha na afya njema ya kiroho.
8. Mfundishe mlevi jinsi ya kupokea nguvu za Mungu kila siku. Mpe moyo wa kusoma Biblia na kuomba kila asubuhi na jioni.
9. Msaidie kupata marafiki wapya ambao hawanywi pombe. Anaweza kusaidiwa sana na rafiki Mkristo mmoja au zaidi ambao wao wenyewe walikuwa walevi lakini baadaye wakaacha kunywa pombe.

Yale Biblia Inayosema Kuhusu FURAHA:

Msomee na umweleze mtu asiye na furaha vifungu hivi:

- Nafsi yangu, kwa nini kuinama, na kufadhaika ndani yangu? Umtumaini Mungu; kwa maana nitakuja kumsifu, aliye afya ya uso wangu, na Mungu wangu; Nafsi yangu imeinama ndani yangu, kwa hiyo nitakukumbuka (Zaburi 42:5-6).
- (Yesu akasema) "Njoni kwangu, ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).
- Msijisumbue kwa neno lo lote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu (Wafilipi 4:6).
- Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na tuwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo (Warumi 5:1).
- Basi Mungu wa tumaini na awajaze ninyi furaha yote na amani katika kuamini, mpate kuzidi sana kuwa na tumaini, katika nguvu za Roho Mtakatifu (Warumi 15:13).
- Maana nimejifunza kuwa radhi na hati yo yote niliyo nayo (Wafilipi 4:11).
- Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu, ndani ya Kristo Yesu (Wafilipi 4:19).
- Hata sasa hamkuomba neno kwa jina langu; ombeni, nanyi mtapewa; furaha yenu iwe timilifu (Yohana 16:24).
- Unirudishie furaha ya wokovu wako; unitegemeze kwa roho ya wepesi (Zaburi 51:12).

Vifungu vingine ambavyo mnaweza kusoma ni:

Zaburi 51:1-2	Yohana 15:10-11
Zaburi 103:1-5	Yohana 16:32-33
Zaburi 102:1-2	1 Wathesalonike 5:16-18
Mathayo 5:12	Yakobo 4:8

Tazama pia katika kitabu hiki: "Huzuni" na shinda nyingine zinazohusiana katika orodha, ukurasa wa 5.

"NDOA YETU INA SHIDA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Ujue ya kwamba wewe peke yako huwezi kutatua shida za ndoa. Lengo lako liwe ni kuwasaidia mume na mke kujitatulia shida zao wenyewe.
2. Jaribu kuwatuliza kwanza, ili uweze kujua jinsi shida ilivyotokea na sababu zake.
3. Fanya uwezavyo ili uweze kuwaona mume na mke pamoja. Msaidie kila mmoja wao kujua ya kwamba wote wawili wamesababisha shida iliyo kati yao wawili.
4. Wasaidie mume na mke kujua shida zenyewe katika ushirika wao wa ndoa.
5. Sikiliza shida hizo bila kupendelea mume wala mke.
6. Toa mashauri kuwasaidia mume na mke ili kuweza kukabiliana na shida za kila siku. Kwa mfano, mshauri kila mmoja wao amfanyia mwenzake mambo mema kila siku.
7. Washauri waombeane, na hata kuomba pamoja kama wao ni Wakristo.
8. Uwe tayari kutumia wakati wako kwa kuijenga upya ndoa iliyovunjika. Washauri mume na mke kuzungumza nawe mara kadhaa zaidi. Shirikiana nao ili mweze kufikia lengo la ushirikiano mwema uletao ndoa yenye furaha.
9. **Usimwambie mwingine habari za shida za watu hawa.**

Yale Biblia Inayosema Kuhusu UMASKINI:

Maelezo kamili kuhusu vifungu hivi yaweza kuwa msaada wakati unapowashauri wale walio maskini.

- Kwa maana mhitaji hatasahauliwa daima; matumaini ya wanyonge hayatapotea milele (Zaburi 9:18).
- Nami ni maskini na mhitaji, Bwana atanitunza. Ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu, Ee Mungu wangu, usikawie (Zaburi 40:17).
- Heri kuchagua jina njema kuliko mali nyingi: Na neema kuliko fedha na dhahabu (Mithali 22:1).
- Maskini na wahitaji wanatafuta maji, wala hapana; ndimi zao zimekauka kwa kiu; mimi Bwana, nitawasikia, mimi, Mungu wa Israeli, sitawaacha (Isaya 41:17).
- Akainua macho yake akawatazama wanafunzi wake, akasema, Heri ninyi mlio maskini, kwa sababu ufalme wa Mungu ni wenu. Heri ninyi mlio na njaa sasa, kwa sababu mtashiba. Heri ninyi mliao sasa, kwa sababu mtacheka (Luka 6:20-21).
- Bwana hataiacha nafsi ya mwenye haki ife na njaa; Bali tamaa ya mtu mwovu huisukumia mbali. Atendaye mambo kwa mkono mlegevu huwa maskini; Bali mkono wake aliye na bidii hutajirisha (Mithali 10:3-4).
- Basi tukaujenga ukuta; nao ukuta wote ukaungamanishwa kiasi cha nusu ya kimo chake; maana watu walikuwa na moyo wa kufanya kazi (Nehemia 4:6).
- Tena mjitahidi kututia, na kutenda shughuli zenu, na kufanya kazi kwa mikono yenu wenyewe, kama tulivyowaagiza (1 Wathesalonike 4:11).
- Basi ikiwa ninyi, mlio waovu, mnajua kuwapa watoto wenu vipawa vyema, je! si zaidi sana Baba yenu aliye mbinguni atawapa mema wao wamwombao? (Mathayo 7:11).

Tazama pia katika kitabu hiki: "Kukosa kazi" na "Huzuni," katika orodha, ukurasa wa 5.

“TWAHITAJI CHAKULA NA PESA.”

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Jaribu kugundua kama kweli wana shida ya chakula na pesa. Baadhi ya watu wanaosema wanayo shida hiyo, kwa kweli huwa hawanayo.
2. Kwa upande mwingine, umaskini kabisa huwa na uchungu. Kwa hivyo ni lazima uwasikilize kwa makini wale ambao wanakuja ili kupata msaada.
3. Makanisa mengine hupendelea kuwa na kamati maalum za kuchunguza kila mahitaji. Kamati ndiyo huamua na ni hasa anayehitaji msaada. Kamati hiyo inaweza kutumia michango maalum ya kanisa au chakula ambacho kimekusanywa kwa ajili ya maskini. Pia ingewezekana kuwapatia kazi za kibarua wafanye ili waweze kujisaidia zaidi.
4. Wewe, kama kiongozi wa kanisa, unaweza kusaidia zaidi kwa kuwaongoza watu waelewe kinachosababisha umaskini. Hii inaweza kuwa nafasi nzuri ya kufundisha kwa kifupi juu ya kufanya kazi kwa bidii na matumizi ya pesa mtu alizo nazo.
5. Kiini cha umaskini kinaweza kuwa tabia mbaya kama ulevi. Katika hali kama hiyo, fuata mashauri yaliyotolewa mahali pengine katika kitabu hiki. Kwa mfano, tazama: “Mume wangu hunywa pombe sana.” (Ukurasa wa 30).
6. Waulize jamaa jinsi wanavyofikiria juu ya mahitaji hayo. Mara nyingi baadhi ya jamaa wanaweza kusaidia wakiwa wameelewa shida yenyewe.
7. Inakupasa wewe mwenyewe uwaulize baadhi ya washiriki wa kanisa kama kuna kazi yo yote inayoweza kupatiwa yule aliye na shida.
8. Ikiwa njaa imeenea kila mahali, baada ya ukavu au mafuriko, unahitaji kutafuta jinsi utakavyopata msaada kutoka kwa serikali au misheni.
9. Yapasa kanisa lako kushirikiana katika mipango ya jamii au ya serikali yenye lengo la kuzuia njaa. Hii inaweza kuwa ukuzaji wa mimea ya chakula, kuhifadhi maji au nafaka, ukuzaji wa mazao ya kuuza, usitawi wa sanaa, n.k.

Yale Biblia Inayosema Kuhusu NDOA:

Tumia vifungu hivi wakati unapowasaidia watu walio na shida katika ndoa zao.

- Uchungu wote na ghadhabu na hasira na kelele na matukano yaondoke kwenu, pamoja na kila namna ya ubaya; tena iweni wafadhili ninyi kwa ninyi, wenye huruma, mkasameheane kama na Mungu katika Kristo alivyowasamehe ninyi (Waefeso 4:31-32).
- Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine (Wafilipi 2:3-4).
- Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake, hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote (1 Wakorintho 13:4-7).
- Ninyi wake, watiini waume zenu, kama ipendezavyo katika Bwana. Ninyi waume, wapendeni wake zenu msiwe na uchungu nao (Wakolosai 3:18-19).
- Ndoa na iheshimiwe na watu wote, na malazi yawe safi; kwa maana waasherati na wazinzi Mungu atawahukumia adhabu (Waebrania 13:4).
- Hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe; maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu (1 Wakorintho 6:19-20).

Vifungu vingine vya kusoma ni:

Ruthu 1:16	Waefeso 5:22-24
Mithali 5:1-4; 15-20	Waebrania 12:4-7
Zaburi 18:22	1 Petro 3:1-6

Tazama pia katika kitabu hiki: “Uasherati,” “Uchungu” na “Watoto.” Tafuta katika orodha, ukurasa wa 5.

"NIMETENDA DHAMBI KUBWA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Anza kwa kusema ya kwamba Mungu yu tayari kusamehe dhambi. Unaweza kusafishwa kabisa dhambi zako zote. Lakini kwanza ni lazima kuelewa zaidi juu ya dhambi na matokeo yake.
2. Uliza ni dhambi au ni makosa ya aina gani yaliyosababisha wasiwasi na hatia. Jaribu kutafuta chanzo cha shida hiyo. Pia jaribu kujua jinsi mtu huyo anavyojisikia kuhusu dhambi zake.
3. Taja ya kwamba kutambua kuwa tumefanya makosa ni hatua ya kwanza ya kushinda dhambi. Kukubali kwamba tumekosa ni kufungua mlango ili neema ya Mungu iingie ndani yetu.
4. Ikiwa yule mtu anayejisikia mwenye hatia si Mkristo, msaidie ili ampokee Yesu kuwa Mwokozi wake. Iwapo dhambi ndiyo shida, suluhisho lake ni wokovu. (Jinsi ya kumwongoza mtu awe Mkristo imeelezwa katika sehemu nyingine ya kitabu hiki. Tazama ukurasa wa 37).
5. Kwa wale ambao ni Wakristo, hatua tano zinazofuata ni muhimu katika kushinda dhambi na hatia.
   - A. TUBU. Soma 1 Yohana 1:9. Toba ni jibu kutoka kwa Mungu. Kujisikia mwenye hatia ni njia ya Mungu ya kusema, "Umekosa." Kutubu ni njia ya kusema, "Ninakubali; Nimekosa." Mwongoze mtu huyo atubu dhambi zake kwa Mungu katika maombi.
   - B. POKEA MSAMAHA WA MUNGU. Soma Waefeso 1:7. Neema ya Mungu ni kubwa zaidi kuliko dhambi zako.
   - C. SAHIHISHA MAKOSA YAKO KWA YULE ULIYEMKOSEA. Soma Mathayo 18:15-16.
   - D. SAHAU KOSA HILO. Soma Wafilipi 3:13. Jisamehe wewe mwenyewe jinsi Mungu alivyokusamehe wewe.
   - E. ENDELEA MBELE. Soma Wafilipi 3:14. Endelea mbele kwa kumsifu Mungu kwa ajili ya utakaso na amani yake. Endelea kwa kujishughulisha kuwahudumia watu wengine.
6. Mkumbushe mtu huyo mwenye dhambi na kujisikia mwenye hatia ya kwamba hatua hizo tano zinaweza kufuatwa katika dhambi, shida au makosa ye yote yatokeapo siku za usoni.

Yale Biblia Inayosema Kuhusu TAMAA na TABIA:

- Hakika Mungu ni mwema kwa hao walio safi mioyo yao. Nami miguu yangu ilikuwa karibu na kupotoka; Hatua zangu zilikuwa karibu na kuteleza (Zaburi 73:1-2).
- Nalikuwa kama mjinga, sijui neno; Nalikuwa kama mnyama tu mbele zako. Walakini mimi ni pamoja nawe daima, Umenishika mkono wa kuume. Utaniongoza kwa shauri lako, Na baadaye utanikaribisha kwa utukufu. Ni nani niliye naye mbinguni, wala duniani sina cha kupendeza ila Wewe. Mwili wangu na moyo wangu hupunguka, bali Mungu ni mwamba wa moyo wangu na sehemu yangu milele (Zaburi 73:22-26).
- Jaribu halikuwapata ninyi, isipokuwa lililo kawaida ya wanadamu; ila Mungu ni mwaminifu; ambaye hatawaacha mjaribiwe kupita mwezavyo; lakini pamoja na lile jaribu atafanya na mlango wa kutokea, ili mweze kustahimili (1 Wakorintho 10:13).
- Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kwa kuwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele (Wagalatia 6:7-8).
- Msijisumbue kwa neno lo lote, bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu. Na amani ya Mungu, ipitayo akili zote, itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Kristo Yesu. Hatimaye, ndugu zangu, mambo yo yote yaliyo ya kweli, yo yote yaliyo ya staha, yo yote yaliyo ya haki, yo yote yaliyo safi, yo yote yenye kupendeza, yo yote yenye sifa njema; ukiwapo wema wo wote, ikiwapo sifa nzuri yo yote, yatafakarini hayo. Mambo mliyojifunza kwangu na kuyapokea, na kuyasikia na kuyaona kwangu, yatendeni hayo; na Mungu wa amani atakuwa pamoja nanyi (Wafilipi 4:6-9).
- Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia (1 Yohana 2:15-16).

"NINA TAMAA KUBWA ZISIZO ZA KIKRISTO."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Eleza ya kwamba tamaa mbaya na nzuri ni mambo ya kawaida kwa watu wote. Kila mtu anayo tamaa ya chakula, upendo, ngono, kulala n.k. Shida hutokea tamaa ipitapo kiasi.
2. Chunguza upate kujua ni tamaa gani hasa zinazosababisha shida. Je, ni tamaa za uzinifu au ni tamaa za pesa? Je, tamaa zimeanza kusababisha tabia mbaya?
3. Baada ya kujua ni tamaa gani zinazoleta shida, dokeza kwamba inapasa tamaa hizo kupewa Mungu katika maombi. Mungu alituumba, kwa hiyo akili zetu na miili yetu ni yake. Roho wa Mungu anaweza kutusaidia kutawala tamaa zetu.
4. Someni pamoja vifungu hivi vitatu: Wakolosai 1:16; Warumi 6:13; 1 Wakorintho 6:12-20. Eleza vifungu hivyo.
5. Panga mpango wa kutafakari maandiko ya Biblia. Hii inaweza kufanya fikira zetu kwenda pamoja na Neno la Mungu. Ukivikariri vifungu maalum vya Biblia, kama vile vilivyomo katika ukurasa unaofuata, utapata nguvu unaposumbuliwa na tamaa ambazo si za Kikristo.
6. **Panga tarehe iwe kama lengo la kuwa huru kutoka katika shida hiyo. Uhuru huo waweza kupatikana kwa msaada wa Mungu na bidii yako baada ya wiki au miezi michache.**
7. **Sasa mletee Mungu tamaa hizo katika maombi. Mhimize mtu mwenye shida hiyo kuomba mara kwa mara kila siku ili aweze kutawala tamaa zake.**
8. **Mtu anapojaribiwa na tamaa ambazo si za Kikristo, mshauri ajiulize maswali haya matatu yafuatayo:**
   - A. **Je, ninaweza kutenda jambo hili kwa utukufu wake Mungu?**
   - B. **Ninaweza kufanya nini badala ya tendo hili?**
   - C. **Je, Yesu angefanya nini kuhusu jambo hilo?**

Yale Mungu Anayosema Kuhusu DHAMBI na HATIA:

Tumia vifungu hivi vikusaidie kueleza juu ya **dhambi, hatia na** msamaha:

- Haya, njoni, tusemezane, asema Bwana. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera, zitakuwa kama sufu (Isaya 1:18).
- Kwa kitambo kidogo nimekuacha; lakini kwa rehema nyingi nitakukusanya. Kwa ghadhabu ifurikayo nalikuficha uso wangu dakika moja, lakini kwa fadhili za milele nitakurehemu, asema Bwana, Mkombozi wako (Isaya 54:7-8).
- Usiku umeendelea sana, mchana umekaribia; basi na tuyavue matendo ya giza, na kuzivaa silaha za nuru. Kama nilivyohusika na mchana na tuenende kwa adabu; si kwa ulafi na ulevi, si kwa ufisadi na uasherati, si kwa ugomvi na wivu. Bali mvaeni Bwana Yesu Kristo, wala msiuangalie mwili, hata kuwasha tamaa zake (Warumi 13:12-14).
- Kwa maana ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo mabaya, uasherati, wivi, uuaji, uzinzi, tamaa mbaya, ukorofi, hila, ufisadi, kijicho, matukano, kiburi, upumbavu. Haya yote yaliyo maovu yatoka ndani, nayo yamtia mtu unajisi (Marko 7:21-23).
- Tubuni basi, mrejee, ili dhambi zenu zifutwe, zipate kuja nyakati za kuburudishwa kwa kuwako kwake Bwana (Matendo 3:19).
- Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi (Warumi 5:8).
- Mimi, naam, mimi, ndimi niyafutaye makosa yako kwa ajili yangu mwenyewe; wala sitazikumbuka dhambi zako (Isaya 43:25).

"BINTI YETU ANA MIMBA, LAKINI HAJAOLEWA."

JINSI YA KUSAIDIA:

1. Mimba kwa wasichana wasioolewa ni shida kubwa inayotokea mara kwa mara. Ni pigo kubwa kwa jamaa ya msichana huyo aliyepata mimba na inaweza kuwa na hasira nyingi.
2. Kusanya habari yote kuhusu hali yenyewe kwa kusikiliza kwa makini. Uliza maswali kama: kumefanyika nini hadi sasa? Kumefanywa nini ili kupata suluhisho?
3. Jaribu kuwapa matumaini. Hii inaweza kufanyika kwa kusema: "Mungu yuko tayari kukusaidia wewe pamoja na binti yako." Soma Zaburi 147:3.
4. Toa mashauri juu ya kutoharibu mimba. Kuondoa uhai wa mtoto ambaye hajazaliwa si suluhisho kutoka kwa Mungu.
5. Epuka kumlaumu msichana peke yake. Baba ya mtoto huyo ambaye hajazaliwa, pia amefanya dhambi. Makosa yamefanywa na wazazi wao pia.
6. Panga wakati wa kuzungumza na msichana anayehusika haraka. Juhudi pia zifanywe ili kuzungumza na baba ya mtoto ambaye hajazaliwa.
7. Usimlaumu msichana huyo mwenye mimba mnapozungumza. Msaidie kujua ya kwamba ametenda kosa kubwa. Na kwa hivyo sasa, anastahili kukubali matokeo yake.
8. Msaidie binti huyo mja mzito kuanza kujitayarisha mapema kuwa mama mzazi. Anastahili kuendelea kuishi maisha ya kawaida kama iwezekanavyo. Kwa mfano, inampasa kuendelea na masomo yake, au atafute mafunzo ya aina fulani. Umalaya si mapenzi ya Mungu
9. Onyesha wazi ya kwamba mtoto atakayezaliwa na msichana huyo asiyeolewa hana makosa yo yote. Awe wa kiume au wa kike anastahili kupendwa na mama yake na jamaa yote kwa jumla.

Yale Biblia inayosema kuhusu DHAMBI za UASHERATI:

Tumia vifungu hivi unaposhauri juu ya uasherati.

- Lakini mwili si kwa zinaa, bali ni kwa Bwana, naye Bwana ni kwa mwili (1 Wakorintho 6:13).
- Basi, dhambi isitawale ndani ya miili yenu ipatikanayo na mauti, hata mkazitii tamaa zake, wala msiendelee kuvitoa viungo vyenu kuwa silaha za dhuluma kwa dhambi; bali jitoeni wenyewe kwa Mungu kama walio hai baada ya kufa, na viungo vyenu kwa Mungu kuwa silaha za haki (Warumi 6:12-13).
- Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele (1 Yohana 2:15-17).
- Bali tukienenda nuruni, kama yeye alivyo katika nuru, twashirikiana sisi kwa sisi, na damu yake Yesu. Mwana wake, yatusafisha dhambi zote. Tukisema kwamba hatuna dhambi, twajidanganya wenyewe, wala kweli haimo mwetu. Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote (1 Yohana 1:7-9).
- Huku mkimtwika yeye fadhaa zenu zote, kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu (1 Petro 5:7).
- Nimeyafuta makosa yako kama wingu zito, na dhambi zako kama wingu; unirudie; maana nimekukomboa (Isaya 44:22).
- Huwaponya waliopondeka moyo, na kuziganga jeraha zao (Zaburi 147:3).

Angalia pia katika kitabu hiki: Uasherati, Mkristo kurudi nyuma, Ndoa na Dhambi. Tazama orodha katika ukurusa wa 5.